

JINA \_\_\_\_\_ NAMBAJI YAKO:\_\_\_\_\_

TAREHE:\_\_\_\_\_

**KAUNTI NDOGO YA GATUNDU**

**MTIHANI WA MAKADIRIO**

**102/2**

**KISWAHILI**

**KARATASI 2**

**LUGHA**

**Julai/Agosti 2016**

**Muda: Saa 2 ½**

**MAAGIZO:**

1. Andika jina na nambari yako katika nafasi iliyoachwa hapo juu.
2. Jibu maswali yote.
3. Maswali yote yaandikwe katika nafasi zilizoachwa katika kijitabu cha maswali.
4. Usitoe ukurusa wowote kutoka kwenye kijitabu hiki.
5. Watahiniwa ni lazima wahakikishe kwamba kurasa zote zimepigwa chapa sawasawa na kuwa maswali yote yamo.

**Kwa matumizi ya Mtahini Pekee.**

SWALI	UPEO	ALAMA
1	15	
2	15	
3	40	
4	10	
	80	

## 1. UFAHAMU (alama 15)

**Soma taarifa hii kisha ujibu maswali yanayofuata.**

Katika kongamano la wataalamu wa lugha lililofanyika jijini Nairobi mnano Septemba mwaka wa 2013, **mwandishi mahashumu**, Prof. Euphrase Kezilahabi wa Tanzania alishangaa kwamba, ingawa Kiswahili ni lugha iliyochangia sana katika kuenea kwa dini, elimu na kufanikisha biashara, Afrika ya Mashariki na kati kwa muda mrefu, haijasaidia kuleta umoja na muumano maridhawa katika eneo hili. Kadhalika, kwenye kongamano hili, wataalamu wawili wa watunzi wapevu wa fasihi ya Kiswahili – Prof. John Hamu Habwe na Prof. Kithaka wa Mberia, wa Chuo Kikuu cha Nairobi walilalamika kwamba, wahakiki wa fasihi kwa muda mrefu wamekuwa wakiipuza fasihi ya Kiswahili na **kuiweka pembezoni** katika taaluma nzima ya wasomi, wanasiasa, wanahistoria na hata wanahabari.

Si swala la mjadala tena kwamba lugha inayofumbata hisia za wenyeji wengi wa Afrika ya Mashariki ni Kiswahili. Ingawa watu wa mataifa haya waligawanywa kwa kuwekewa mipaka na wakoloni kwa minajili ya wakoloni hao kukidhi mahitaji yao ya kisiasa na kiuchumi, kimsingi watu wa eneo hili wana historia na tamaduni zilizokurubiana.

Sina hakika iwapo Prof. Kezilahabi amekwisha kusoma vitabu vitatu ambayo nafikiri vinaweza kujibu swali lake. Vitabu hivyo ni *Swahili State and Society: The Political Economy of an African Language* (Alamin Mazrui na Ali Mazrui), *The Power of Babel* (Mazrui na Mazrui), *Kiswahili: Past, Present and Future Horizons* (Rocha Chimerah), na *Language Policy in East Africa* (Ireri Mbaabu). Katika *Swahili State and Society*, Prof. Ali Mazrui na Prof. Alamin Mazrui wanahoji kwamba ufuasi wa watu katika makabila yao bado ni mkubwa sana Afrika kwa jumla na hasa Afrika ya Mashariki.

Hali hii ilidhahirika katika Uchaguzi Mkuu wa Kenya uliofanyika Machi mwaka wa 2013 – ambapo tuliona watu wakiamini sana vyama vya kisiasa kwa misingi ya ukabila bila kutilia maanani sera za vyama hivyo. Aliyekuwa Waziri Mkuu, Bw. Raila Odinga alikuwa na wafuasi wengi kutoka watu wa kabilia lake, huku Rais Uhuru Kenyatta akiwa na wafuasi wengi kutoka jamii yake ya Agikuyu, naye naibu wake William Ruto akiwa na wafuasi kutoka kwa jamii yake ya Wakelenjin.

Huku Prof. Kezilahabi akiwa ana wasiwasi kwamba Kiswahili bado hakijafanikiwa kuunganisha watu wa Afrika ya Mashariki, Prof. Chimerah ana mtazamo tofauti. Ameipanulia mawanda lugha hii na kuipigia upatu iwe **lingua franca** ya bara la Afrika. Mtazamo wa Prof. Ireri Mbaabu wa Chuo Kikuu cha Kenyatta kuhusu suala hili ni kwamba, mikakati ya kisera kuhusiana na lugha katika mataifa ya Afrika Mashariki ni tofauti. Kiswahili ni lugha ya taifa nchini Tanzania.

Hivi majuzi, serikali ya Kenya ilikikweza hadhi Kiswahili kuwa lugha rasmi sambamba na Kiingereza – licha kwamba bado Kiswahili ni lugha ya taifa. Nchini Uganda, Kiswahili bado hakijapokelewa vizuri kwa sababu kinaendelea kupata ushindani mkubwa kutokana na lugha ya Luganda. Isitoshe, kwa

muda mrefu, Kiswahili nchini humo kimekuwa kikipigwa vita kwa sababu kilihushisha na ukatili wa wanajeshi. Hatua ya Kenya kurasimisha Kiswahili sambamba na Kiingereza ni tamko la kisera.

Hadi sasa, hatujaona hatua za kimakusudi za kulifanyia kazi tamko hili. Kenya, haina chombo rasmi cha kiserikali kinachowezza kutekeleza majukumu ya kuendeleza Kiswahili kimakusudi.

Jukumu hili limeachiwa watu binafsi na vyombo nya habari kama vile gazeti la Taifa Leo. Kuhusu suala la kuwekwa pembezoni kwa fasihi ya Kiswahili na wahakiki wa fasihi wanaozingatia mno fasihi ya Kiingereza, ni hali ya kusikitisha mno. Wasichokifahamu wahakiki hawa ni kwamba, fasihi ya Kiswahili imepiga hatua mno hasa kuhusiana na utunzi wa kimajaribio.

Kwa hiyo, ni upumbavu wahakiki kuifumbia macho fasihi ya Kiswahili ambayo inazidi kupanuka kila uchao. Kimsingi, kinachozua Afrika Mashariki kuungana na kuwa na mshikamano anaoutaka Prof. Kezilahabi ni tofauti za kisiasa, kiuchumi na kisera ambazo hazijawianishwa. Muungano wa Afrika ya Mashariki utakapoimarika, labda ndipo mataifa ya eneo hili yatakapofikia mshikamano wa kuridhisha utakaofanikishwa kwa matumizi ya lugha ya Kiswahili.

**MASWALI:**

- (a) Upe ufahamu huu anwani mwafaka. (Alama 1)

---

---

- (b) Eleza matatizo yanayokumba Kiswahili kwa mujibu wa ufahamu. (Alama 5)

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

- (c) Linganua mitazamo ya Kezilahabi na Chimerah kuhusu Kiswahili. (Alama 2)

---

---

---

---

---

- (d) Kwa nini mwandishi anadai kuwa hatua ya Kenya kurasimisha Kiswahili sambamba na Kiingereza ni tamko la kisera. (Alama 2)

---

---

---

---

- (e) Eleza sababu za kuonyesha kuwa haifai wahakiki wa fasihi kupuuza fasihi ya Kiswahili. (Alama 2)

---

---

---

---

- (f) Eleza maana ya vifungu vifuatavyo kwa mujibu wa ufahamu. ( Alama 3)

(i) Mwandishi mahashumu

(ii) Lingua franca

(iii) Kuweka pembezoni.

---

## 2. UFUPISHO (ALAMA 15)

**Soma makala yafuatayo kisha ujibu maswali.**

Kuna sababu kadha za kuwako na kushamiri kwa ajira ya watoto. Moja ya sababu hizo ni umaskini unaozikumba jamaa nyingi pamoja na *welewa* mdogo wa thamani ya elimu wa baadhi ya watu katika jamii. Wapo watoto ambao hushurutika kubeba jukumu la *kujizumbulia* riziki wenyewe kutokana na hali duni ya familia zao.

Hali hii huweza kutokana na baadhi ya wazazi *kutelekeza majukumu* yao ya kimsingi ya kuikimu jamaa yao. Aidha kuna sehemu nyingine ambapo hali hii imetokana na janga sugu la ukimwi. Yapo maeneo ambako kuenea kwa ugonjwa huu kumewafanya viongozi wa jamaa *kupukutika kama majani* ya mti na kuwalazimisha watoto kuyakatiza masomo yao ili wawakidhie haja wadogo zao. Kuhusiana na kutelekeza majukumu, kuna wazazi ambao wanakosea kwa kutowaelekeza watoto wao kujua maadili mema ni yepi. Kwa njia hii watoto hao wanaishia kutumbukia kwenye matatizo makubwa.

Baadhi ya ajira zina athari kubwa sana kwa watoto. Ukahaba, kwa mfano, ni mojawapo ya ajira ambazo watoto wa kike hulazimika kuijingiza. Hii ni ajira ambayo inaweza kuwatumbukiza watoto hao katika hatari kubwa kutokana na uwezekano mkubwa wa kuambukizwa maradhi ya ukimwi. Asillimia kubwa ya watoto wanaotumbukia katika ajira hii, inapatikana katika maeneo ya mijini na sehemu ambako utalii umeshamiri sana. Umaskini pamoja na dhiki za mijini huwalazimisha watoto hao wa kike kuishia kwenye biashara za aina hiyo. Wengine hufanyiwa hila na wafanyabiashara ambao *wametovukwa na utu* kutokana na tamaa yao kubwa ya kujitajirisha. Katika maeneo ambako utalii umeshamiri, ukahaba wa watoto unatokana na umaskini pamoja na kusambaa na kuenea kwa *maadili ajinabi*, ya ulimwengu usio wetu.

Ikiwa umaskini ni chocheo kubwa la kuwapo kwa ajira ya watoto, basi inahalisi serikali zetu zifanye kila juhudhi kuhakikisha kuwa umaskini umepigwa vita. Pana umuhimu wa kuhakikisha kuwa wanajamii wote wamepewa nafasi sawa za *kujikwamua kutoka lindi la umaskini*. Isitoshe, pana umuhimu wa juhudhi nyingi kufanywa kuhakikisha kuwa nafasi za shule zimepanuliwa ili kuikidhi idadi kubwa ya watoto ambao wana kiu ya elimu. Serikali haina budi pia kuhakikisha kuwa zimepitishwa sheria zinazomlinda motto dhidi ya ukatili unaotokana na watu waliokosa hisia za utu na ubinadamu. Upo pia umuhimu wa kuvisaidia vikundi vinavyojitahidi kuwasaidia watoto ili kuzifanikisha juhudhi zao kwa kuwa chanda kimoja hakivunji chawa kama tujuavyo.

Hatua nyingine ambazo zinaweza kuchukuliwa ili kupunguza ajira ya watoto ni *kuwahamasisha wanajamii* kuhusu haki za mtoto. mtoto yelete yule ana haki ya kupata elimu ya msingi. Mtoto pia ana haki ya kuishi na kupata mahitaji ya kimsingi na ya lazima kama chakula, malazi au makazi na matunzo ya kiafya. Aidha mtoto ana haki ya ukuaji, yaani kukua kikamilifu pasi na kizuizi na katika mazingira yasiyombana kwa njia yoyote ile. Isitoshe, mtoto ana haki ya kupata ulinzi dhidi ya unyanyaswaji au udhalilishwaji wa aina yoyote ile au hata maonevu kwenye misingi yoyote iwayo. Mtoto pia ana haki ya kuwa huru kushiriki katika jumuiya yake, kutoa maoni na kujieleza, kushirikiana na kujiunga na vikundi. Mwisho, na muhimu zaidi, mtoto ana haki ya kulindwa dhidi ya ajira au aina yoyote ya kazi ambayo inaihatarisha afya na siha yake au inamzuia asipate elimu.

(a) Fupishaaya mbili za mwanzo bila kubadilisha maana.

**Matayarisho:** (maneno 60-70) (alamu 7) alamu 1 mtiririko.

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

**Jibu**

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

(b) Eleza hoja muhimu zinazojitokeza katika aya mbili za mwisho. (Maneno 50-60) (alamu 6)  
(Alamu 1 utiririko.)

Matayarisho:

Jibu:

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

### **3. MATUMIZI YA LUGHA: (ALAMA 40)**

(a) Taja vitamkwa vyenye sifa zifuatazo. (Alama 2)

(i) Vokali ya nyuma, kati.

---

(ii) Nazali ghuna ya midomo.

---

(b) Kiambishi ni nini? Alama 2

---

---

(c) Unda kitenzi chenye mofimu hizi. (Alama 3)

(i) Nafsi ya tatu umoja.

(ii) Kiambishi cha wakati uliopita.

(iii) Kirejeshi.

(iv) Kiambishi cha mtendewa.

(v) Mzizi wa kitenzi.

(vi) Kiishio.

(d) Tumia kitenzi “amerudi” kuonyesha dhana ya tatu za kiimbo. (Alama 3)

---

---

---

---

(e) Tambua hali katika sentensi ifuatayo.

Vyungu vya aina hii vyafinyangwa na huyu. (Alama 2)

---

---

(f) Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizowekwa katika mabano. (Alama 2)

(i) Lia (kutendeshwa) \_\_\_\_\_

(ii) Pa (kutendea) \_\_\_\_\_

(g) (i) Eleza maana ya mzizi. (Alama 1)

---

---

(iii) Toa mfano wa:- (Alama 2)

Mzizi huru \_\_\_\_\_

Mzizi fungo \_\_\_\_\_

(h) Andika katika hali ya ukubwa.

Kigombe kile kiliumia kwato. (Alama 2)

---

---

(i) Eleza matumizi mawili ya “ka”. (Alama 2)

---

---

---

---

---

---

(j) Onyesha aina za virai katika sentensi hii. (Alama 3)

Wazazi wetu watawasili kesho saa tatu.

---

---

- 
- 
- 
- (k) Onyesha kiima na kiarifa katika sentensi ifuatayo. (Alama 2)  
Wanafunzi watakaolala darasani wataadhibiwa vikali.
- 
- 
- 

- (l) Onyesha shamirisho katika sentensi ifuatayo. (Alama 3)  
Wanafunzi walikatiwa keki na mwalimu kwa kisu.
- 
- 
- 

- (m) Changanua sentensi ifuatayo kwa njia ya jedwali. (Alama 3)  
Sisi tulipokuwa shulenii tulisoma kwa bidii.
- 
- 
- 
- 
- 

- (n) Onyesha matumizi mawili ya kibainishi katika sentensi. (Alama 2)
- 
- 
- 
- 
- 

- (o) Andika sentensi hii katika usemi wa taarifa. (Alama 2)  
“Tutakuja kwenu leo”. Mama alisema.
- 
- 
- 
- 
-

(p) Unda nomino mbili kutohana na neno “kudhulumu”. (Alama 1)

---

---

---

(q) Tambua miundo yoyote mitatu ya nomino za ngeli ya A-WA kwa kutoa mifano. (Alama 3)

---

---

---

---

**4. ISIMU JAMII. (alama 10)**

(a) Fafanua sababu zozote nne zinazosababisha makosa katika matumizi ya lugha. (Alama 4)

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

(b) Eleza nadharia zozote mbili zinazoelezea chimbuko la Kiswahili. (Alama 4)

---

---

---

---

---

---

---

---

---

---

- (c) Eleza mambo mawili yanayosababisha kufa kwa lugha. (Alama 2.)

---

---

---

---

---